

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram "AFYA", DODOMA
Namabari ya Simu: +255 026 – 2323267



Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya
S.L.P. 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

Dar es Salaam, Jumatatu Aprili 13, 2020

Wizara inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa **kumi na nne (14)** wa Corona (COVID-19) nchini hadi kufikia 46 kutoka 32 tuliowatolewa taarifa ya awali tarehe 10 Aprili, 2020.

Wagonjwa wapya 14 wote ni Watanzania. Kati ya hawa Wagonjwa walioko Dar es Salaam ni 13 na mmoja yuko Arusha. Wagonjwa wote wanaendelea na matibabu chini ya uangalizi wa wataalam wa afya. Ufuatiliaji wa watu waliokuwa karibu na wagonjwa unaendelea.

Kwa mara nyingine Serikali inarudia tena kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kama tunavyowapatia taarifa na elimu mara kwa mara kupitia njia mbali mbali na hususan kuepuka misongamano na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima.

Handwritten signature of Umy Mwalimu in black ink.

Umy Mwalimu (Mb)
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**